

Ni mchana tulivu katika jiji la Nairobi Flaviana alikuwa amejifungia ndani kwenye chumba kilichokuwa kidogo na chenyé madarisha makubwa yalio pitisha mwanga angavu.

Flaviana alifikili kupita kiasi alikuwa amekaa kwenye stuli mbele ya kiti chake alikuwa ameweka meza ndogo iliyokuwa na daftali kubwa mkononi.

Alishikilia karamu anakua makini anakuna kichwa chake akifikilia mambo mengi kuhusu kazi yake ya uwandishi kazi iliyomchukua muda mwingi kuifikilia ni kwa namna gani atawenza kuifanya ilete tija kwenye maisha yake.

Flaviana alikuwa binti yatima wazazi wake walikufa katika vita kubwa iliyozuka Nchini Sudan katika mji wa Kartoum Flaviana alizaliwa nakukulia Sudan alisoma masomo yake shule ya msingi hadi sekondari katika mji wa Kartoum,

"Dah nimechoka" anaongea mwenyewe huku akijinyoosha alichoka mwili mzima kwakuwa tangu anaamka asubuhi aliamkia kuandika kitabu chake ambacho kilimchukua akili nyingi anafungua mlango na kutoka nje anaacha karamu na daftali lake alinyoa nywere zake.

Anapotoka nje anakutana na rafiki yake UPendo aliyekuwa akiishi nae kwenye nyumba isiyo tamanika illiyokuwa pemberi mwa chumba alichokuwa amekaa, "Flaviana tunakula nini?" anauliza upendo.

"Nina kiasi kidogo cha fedha" anazungumza kwa sauti ya unyenyekevu huku akitoa pesa katika mfuko wake wa sketi upatikanaji wa fedha ulikuwa mgumu kwa mabinti hao wawili.

Upendo alikuwa ni muimbaji na mtunzi wa nyimbo za injiri na mpigaji wa vyombo vya muziki zilikuwa ni karama ambazo Mungu alimtunukia,

"Badae nitaenda kwenye tamasha la ukombozi, watanilipa fedha nyingi" anasema Upendo akimuondoa wasiwasi rafiki yake, "Mimi nitaenda kiwanda cha kuchapisha vitabu nakazi naenda kufanya" wanapeana taarifa zilizo njema.

Upendo alikuwa ni Raia halisi wa Kenya nae alipoteza wazazi wake akiwa na umli wa miaka tisa aliishi nakusomeshwa na kituo cha watoto yatima baada ya kufikisha umli wa miaka 17 anafukuzwa kituoni ndipo alianza maisha ya kujitegemea mwenyewe mtaani,

"Ngoja nika nunue unga na mboga tujetupike" anasema upendo huku akiondoka kuelekea sehemu kulipokuwa na soko dogo la mtaa, "Natakiwa kufika mbali, nitafika vipi?" anajiuliza maswali mengi kichwani uwezo wake katika kuandika vitabu ulikuwa mkubwa alifahamu lugha ya Kiswahili na kингereza vyema.

"Lakini nitafika" anawaza huku akivuta hisia za matarajio yake aliyokuwa nayo akitaka kuwa mwandishi nguri Afrika ya mashariki,

Walikuwa na mwaka mmoja wakiwa wanaishi pamoja na upendo waliyaanza maisha wakiwa wote wawili Flaviana akitokea katika kambi za wakimbizi akiwa ametoroka na kugushi uraia wa Kenya.

Document zake zilionyesha mkenya kilicho mbeba alijuwa lugha ya Kiluya kwa sifa hizo chache ziliwafanya watu wengi kujuwa kwa haraka ni mkenya aliyekuwa akijuwa siri hiyo nzito kuhusu Flaviana ni Raia wa Sudan alikuwa Upendo pekee,

Anapofika soko lile dogo la mtaa anakutana na waimba kwaya wa kanisa lake wanamchangamkia, "Upendo usiache kuja, mpiga gita hayupo" yalikuwa maneno yenye msisitizo kuonyesha umuhimu wa Upendo.

"Nilazima nije atapastor aliniambia nije" anasema upendo akiwa nimwenye uchangamfu, "fedha ipo kanisa litakulipa" anaendelea kuhakikishiwa kila kitu kitaenda vyema alikuwa mahili akikodiwa hata nje ya kanisa lake.

Upendo alitunga nyimbo zenyenye masifu na utukufu mbele za Mungu, "Unaenda wapi sasa hivi?" wanamuuliza kwakumchangamkia,

Upendo anawajibu "Naenda kununua unga" anaongea akiwa nimwenye amani ya Rohomtakatifu ikitawala ndani ya moyo wake wanaondoka huku wakimuacha na kumsisitiza "Usichelewe" wanaondoka na kuendelea na shughuli zao.

*